Kikongwe

(1)

Baada ya muda mrefu wa huzuni Bwana huyu alichomoa karatasi na akaandika:

“Mpenzi Katarina mimi naondoka na sirejei kamwe! Nitamaliza matatizo yangu ambayo yamenizonga. Nakwambia wazi wazi! Naomba uniwiye radhi nawaomba watoto nao waniwie radhi.”

Na huyo akaondoka pale na kwenda zake.

Alikuwa anasitasita licha ya kuwa alikuwa anajiuliza kimoyomoyo mara nyingi hakuwa na ufumbuzi wa matatizo yake zaidi ya kujitoa uhai. Alikuwa anatembea kwa hatua ndogo ndogo akiwaza rohoni: “Hivi kweli mimi ni mgonjwa.” Daima, Katarina, anasema hivyo, akiwa ananishauri niwe mwenye imani na myakinifu. Hayo karejea mara nyingi.

Pambana na maradhi ya wasiwasi, Joji wala usikate tamaa.

Na hata baba yake alikuwa anamwona kuwa anaumwa, alisema hayo na kumwambia kuwa maradhi hayo ya kurithi yametoka kwa upande wa mama yake. Na Kakhi, mkuu wake wa kazi amempa nasaha mara nyingi ili Joji atulie na ajiweke sawa. Bwana huyo ambaye ni Myahudi akimsemesha kama nduguye akisema mara nyingi huku anatabasamu na kumtania.

Kipenzi changu Joji, nisikilize, wewe unajishughulisha nafsi yako bila faida yo yote ya yale unayoyawaza hayakuongezi kitu cho chote, tatizo kubwa ni kuwa fikra hizo zinakuzuwia na unashindwa kutumia uhai wako vema.

Joji sasa ana miaka thelathini na nane, alimwoa Katarina ambaye ni Mwingereza mwenziwe. Lakini Katarina ana asili ya kutoka India. Ndoa yao imedumu kwa miaka kumi ambayo walipata watoto watatu; wa kwanza Maria (huyo angelikuwa na umri wa miaka kumi, lakini alifariki akiwa na miaka saba); Maiko (ana miaka minane) na Sali (ana miaka sita). Tangu alipofariki mtoto wake wa kwanza – Maria hajatulia. Daima amekuwa mwenye kuwaza tu nini maana ya maisha, nini mauti na sababu gani mpakaapende fikra za falsafa.

Alizidisha maswali sana. Joji alizama katika kusoma falsafa na historia na akawa anasoma dini mbalimbali. Huenda usomaji wake huo mwingi ulimfanya asione ugumu kumwoa KatarinaMkatoliki, mwalimu wa mambo ya dini.

https://www.path-2-happiness.com/sw/simulia-ya-njia-ya-saada-kikongwe

www.path-2-happiness.com/sw